

# Chanjo ya COVID-19: Nakala ya Unayopaswa Kutarajia

Ikiwa unapokea au unanua kupokea chanjo ya COVID-19, unapaswa kujua yafuatayo kabla ya kupokea chanjo.

Chanjo hii ni salama na itasaidia kukulinda dhidi ya COVID-19. Huwezi kuambukizwa COVID-19 kutoka kwa chanjo.

Chanjo haina kemikali ya kuizuia kuharibika. Unaweza kutembelea tovuti ya Idara ya Afya ya Minnesota upate maelezo zaidi kuhusu viungo vya chanjo.

Kila mmoja atapokea chanjo bila malipo yoyote. Hatutazingatia hali yako ya bima na uhamiaji.

Utakapowasili kwenye kituo chako cha chanjo, utapokea maelezo ya ukweli kuhusu chanjo. Utaombwa kuandika jina lako kwenye baadhi ya vituo ili kuthibitisha kuwa ulipokea maelezo ya ukweli na ulikubali kupokea chanjo. Mhudumu wa afya atakuuliza maswali machache ili kuhakikisha kuwa UNASTAHIKI kupokea chanjo.

Anayekupa chanjo atakujulisha ikiwa utahitaji dozi nyingine. Ikiwa unahitaji dozi mbili, unapaswa kuzipokea zote na sharti ziwe za aina moja ya chanjo. Utahitajika kusubiri kwa muda wa wiki tatu hadi nne kabla ya kupokea dozi ya pili.

Baada ya kupokea chanjo, utasubiri kwenye kliniki kwa muda wa takriban dakika 15 hadi 30 ili uhakikishe kuwa huna athari zozote mbaya za mizio. Utakabidhiwa kadi itakayoonyesha tarehe uliyopokea chanjo. Tarehe ya miadi inaweza kuandikwa kwenye kadi, ili uweze kujua siku unayopaswa kurejea ikiwa utahitaji dozi ya pili.

Baada ya kupokea chanjo, unaweza kuwa na athari chache zisizokusudiwa. Athari zisizokusudiwa ni pamoja na maumivu kwenye sehemu uliyodungwa sindano ya chanjo, uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya mwili, homa ya joto au baridi kali. Athari hizi zisizokusudiwa zinapaswa kuisha ndani ya siku moja au mbili. Ni jambo la kawaida kuhisi athari hizi zisizokusudiwa na zinaashiria utendakazi wa chanjo! Ni jambo la kawaida pia kutoshuhudia athari zozote zisizokusudiwa. Ikiwa utaathiriwa sana na mizio baada ya kuondoka kwenye kliniki ya chanjo, piga simu kwa 911, au utembelee hospitali iliyo karibu nawe.

Hata baada ya kupata chanjo ya COVID-19, inabidi uzingatia kanuni zilizowekwa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo ya COVID-19 tembelea: [health.mn.gov/covidvaccine](https://health.mn.gov/covidvaccine)

Minnesota Department of Health  
Communications Office  
PO Box 64975  
St. Paul, MN 55164-0975  
651-201-4989  
[health.communications@state.mn.us](mailto:health.communications@state.mn.us)  
[www.health.state.mn.us](http://www.health.state.mn.us)

24/2/21 (Swahili)

Ili upokee maelezo haya katika muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989